

# **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## **WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI**



### **MALENGO YA MILENIA YANATEKELEZWA KWA KASI NA TANZANIA – UNDP**

“Tanzania imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa Malengo ya Milenia (MDG) 2015 na takwimu zilizotolewa hivi karibuni zinaonyesha nchi imepata mafanikio makubwa katika sekta ya elimu, ambapo idadi na uwiano kati ya watoto wa kike na wakiume wanaotakiwa kwenda shule imeongezeka.” Haya yamesemwa na Bi. Hellen Clark, ambaye ni Mwenyekiti na Mtawala Mkuu na Msimamizi wa Miradi ya Maendeleo, ya Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Akizungumza na waandishi wa habari, Bi. Clark alieleza kuwa Shirika la Mpango wa maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) limeridhishwa na namna Serikali ya Tanzania inavyofanya jitihada katika kutekeleza Malengo ya Milenia (MDG) katika kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2015, hususan malengo yale yanayosisitiza uwezeshaji wanawake na elimu.

“Ufadhili unaotolewa na UNDP hapa Tanzania umeleta mabadiliko makubwa katika kutekeleza mipango mbalimbali. Kwa upande wa elimu ya msingi Tanzania imepiga hatua kubwa, watoto

wengi wameweza kwenda shule, uandikishaji watoto wanaopaswa kwenda shule umeongezeka kufikia asilimia 100. Uwiano kati ya wasichana na wavulana umeongezeka , tofauti na siku za nyuma ambapo idadi kubwa ya wanaokwenda shule ilikuwa ni wavulana''. Alieleza Bi. Clark.

''Ninaamini Malengo ya Milenia yatafikiwa kwa kuwa Tanzania inaendelea katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya uchumi, kutokana na nchi kufanya mabadiliko ya sera zinazotoa nafasi ya kutekeleza na kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia, na hivyo kuleta mafanikio makubwa kabla ya mwaka 2015'' alisema.

Kuhusu uwezeshaji wanawake, Bi. Clark alisema Tanzania imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuwawezesha wanawake kushika nafasi na nyadhifa mbalimbali za juu za uongozi.

Awali, Bi. Clark alikutana na kufanya majadiliano na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mhe. Mustafa H. Mkulo (Mb) kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika kutekeleza Malengo ya Milenia hususan kutokomeza ugonjwa wa Ukimwi, Kuwawezesha wanawake na uandikishaji watoto katika elimu ya msingi.

**Imetolewa na Msemaji Mkuu**

**Wizara ya Fedha na Uchumi**

**13/05/2010**